

FOMU YA MKATABA WA UJENZI

A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA

1	MWAJIRI	Mkurugenzi wa Kanda VETA KANDA YA KATI. S. L. P 2084 Dodoma - Tanzania
2	JINA NA ANWANI YA FUNDI MKUU (<i>Mwajiriwa</i>)	Jina: ROBERT E. KASSIKI Anwani: Dodoma Simu: 0653.800.637... Account number 51710045.980
3	ENEO LA UJENZI	IKUNGI -DVTC All Blocks
4	MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI	KUCHIMBA NA KUJENGA CHEMBA ZA MAJISAFI NA TAKA
5	GHARAMA YA UFUNDI	TSH: 3,165,000/-
6	MUDA WA MKATABA (Tangu Kusainiwa kwa Mkataba):	Tarehe ya Kusaini 27/06/2022 Muda: 8 (Siku) Tarehe ya Kuanza Kazi 27/06/2022 Tarehe ya Kumaliza Kazi 15/07/2022
7	MASHARTI YA MALIPO:	<ul style="list-style-type: none"> Hakuna Malipo ya Awali Fundi atalipwa kwa awamu 3 baada ya kazi husika kukamilika na kukaguliwa

MASHARTI YA JUMLA MKATABA

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vyakie ujenzi kam mchaganga,kokoto,nondo,cement,mbao,marine n.k kulingana na maelekezo ya Mtaalamu Mshauri. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.
2. Fundi mkuu atalazimika kuja na vifaa vyake vyakie kifundi na usalama eneo lake la kazi kama; refrector,panga,sururu,chepe,ndoo,jembe,safety boot,kofia ngumu n.k
3. Fundi mkuu atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.
4. Fundi mkuu asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.
5. Fundi mkuu atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.
6. Fundi mkuu kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.
7. Fundi mkuu atahusika na vitendo (*kama wizi, uharibifu wa mali za chuo*) vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu ye yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.
8. Fundi mkuu kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.
9. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Miezi Mitatu baada ya kazi kukamilika (*Retention Money*) na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.
10. Fundi mkuu ahakikishe anamafundi wasaidizi wasiopungua.....kila siku
11. Ucheleweshaji wa Kazi:
 - Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.

12. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:

- Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri (*kutokana na fedha au vifaa*), Fundi ataongezewa muda wa kumalizia kazi.

13. Uvunjwaji wa Mkataba:

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi mkuu au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi mkuu au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.
- Mkataba utavunjwa endapo fundi mkuu atashindwa kuajiiri mafundi wasaidizi kulingana na ukubwa wa kazi,kama itakavyo elekezwa na washauri,ama kamati.
- Mkataba utavunjwa endapo fundi hatazingatia nidhamu ya kazi,atasababisha vurugu ,taharuki ,migomo ama ugomvi eneo la kazi.
- Mkataba utavunjwa endapo 80% ya mafundi wasaidizi hawatakuwa na Imani na fundi mkuu.

14. Hakutakuwa na ongezeko la gharama zitakazotokana na ongezeko la muda wa mkataba.

MWAJIRI:

Saini: *JKR*

Jina: *John R. Lewanya*

Cheo: *RD*

Tarehe: *27/06/2022*

FUNDI/KIBARUA

Saini: *Rasit*

Jina: *ROBERT E. ITASSIKI*

Cheo: *Fundi*

Tarehe: *27/06/2022*

SHAHIDI WA MWAJIRI

Saini: *John*

Jina: *John Thomas*

Cheo: *Msimwi/21*

Tarehe: *28/06/2022*

SHAHIDI WA FUNDI /KIBARUA

Saini: *Dandi*

Jina: *Dandi J. Mwitu*

Cheo: *Msimwi wa Sait*

Tarehe: *28/06/2022*